



**UMOJA - ONE**
**UN in Tanzania**

Toleo La. 78
Mei- Juni 2018

# Makamu wa Rais awa Mgeni Rasmi Siku ya Mazingira Duniani



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan (katikati) na Waziri anayehusika na Maingira, Mh. January Makamba (kulia kwake) akikagua ukuta wa baharini mara baada ya kuuzindua.
**PICHA | Ofisi ya Makamu wa Rais**

## Vidokezo

- UN kuimarisha ubunifu wa vijana, na kushika nafasi ya kwanza katika maonyesho ya Sabasaba.
- Wahariri kutembelea miradi ya UN.
- Siku ya Wakimbizi Duniani

Kila Juni 5, watu kote duniani wanasherehekea Siku ya Mazingira Duniani (WED). Mwaka huu, akimwakilisha Rais wa Tanzania, Mh. John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wa Rais wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan, aliongoza maadhimisho hayo nchini Tanzania chini ya ujumbe mkuu 'Mkaa ni aghali, tumia nishati mbadala'. Makamu wa Rais alizindua ukuta ulio kandokando ya bahari uliofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) na kutekelezwa na  Ofisi ya Huduma za Miradi ya Umoja wa Mataifa (UNOPS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Ukuta huo wa kando mwa bahari uko katika Barabara ya Barack Obama jijini Dar es Salaam na ulijengwa kwa makusudi ya kuhifadhi ukingo wa bahari hasa kufuatia kuongezeka kwa kina cha bahari kwa sababu ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Ukuta huo umesakafiwa vizuri, una taa za kuashiria mafuriko na kuna viti maalumu kwa watu kuketi, jambo linalomaanisha kwamba ukuta utakuwa na mchango mzuri kwa mazingira na uchumi wa eneo hilo.

***Continues on Page 2***

**Kauli ya Serikali:**

***"Pia ningependa kuwashukuru Umoja wa Mataifa, kupitia shirika la mazingira la Umoja wa Mataifa na UNOPS, kwa kusimamia ujenzi wa ukuta."***

**Makamu wa Rais Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, H.E. Samia Suluhu Hassan wakati wa uzinduzi wa ukuta pembezoni mwa barabara ya Barack Obama , Dar es Salaam.**

***From Page 1***



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Samia Suluhu Hassan akipiga picha ya pamoja mara baada ya kuzindua ukuta wa baharini katika Barabara ya Barack Obama katika Siku ya Mazingira Duniani. Kushoto kwake ni Waziri mwenye dhamana ya Mazingira, Mh. January Makamba, na kulia ni Mratibu wa UN Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez. **PICHA | Ofisi ya Makamu wa Rais**

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Makamu wa Rais aliwataka wakaazi wa Dar es Salaam kuutunza ukuta huo na aliishukuru UN na Taasisi ya Dunia ya Mazingira (GEF) kwa kusaidia katika ujenzi huo. “Tuyatunze mazingira ili kwamba mazingira nayo yatutunze. … Ningependa kutumia fursa hii kuwashukuru Taasisi ya Dunia ya Mazingira kwa kugharimikia ujenzi wa ukuta huu nchini Tanzania. Pia ningependa kuwashukuru Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa kwa kutekeleza miradi kama hii na UNOPS kwa kusimamia ujenzi wa ukuta,” alisema wakati wa uzinduzi wa ukuta huo.

Kwa upande wake, Mratibu wa UN Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez, aliipongeza Serikali kwa kuchukua hatua kuhusu tabia ya nchi katika maeneo mengi na alisisitiza ahadi ya UN kuendelea kusaidia mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi Tanzania. “Katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Tanzania inaonyesha utayari wake wa kushiriki katika ajenda ya dunia kuhusu mazingira na kuchukua hatua kukabiliana na changamotokuhusu Mabadiliko ya Tabia ya Nchi,” alisema Bw. Rodriguez. “Licha ya mkaa, uzalishaji wa plastiki ni changamoto kubwa nchini, hatuna budi kufikiri upya kuhusu namna tunavyotumia mkaa na kutumia vyanzo mbadala vya nishati. Vilevile, hatuna budi kufikiri upya kuhusu njia endelevu juu ya namna tunavyotumia plastiki.”

Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) pia lilishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kwa kushiriki katika maonyesho ya teknolojia mbadala zinazokuweza kuwa suluhu kwa mkaa, kuanzia Mei 28 hadi Juni 5, 2018 kwa kuzingatia ujumbe mkuu ‘Mkaa ni ghali, tumia nishati mbadala’.

## Serikali, Umoja wa Mataifa wawaunga mkono wakimbizi




Mkimbizi anayeishi maeneo ya mijini akisimulia historia yake ya maisha katika siku ya maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Duniani jijini Dar es Salaam. **PICHA | Edgar Kiliba/UNRCO**

Muziki, ngoma, sanaa, michezo na maigizo ni miongoni mwa mambo yaliyopamba maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Duniani (WRD) kwa watu waliokuwa katika kambi tatu za wakimbizi (Mtendeli, Nduta na Nyarugusu) mkoani Kigoma na vilevile jijini Dar es Salaam. Maadhimisho hayo ya mwaka huu yalijumuisha maonyesho ya bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na wakimbizi ili kujipatia riziki.

Kote, mkoani Kigoma na jijini Dar es Salaam, sherehe hizo zilihudhuriwa na wakimbizi, watetea haki za kibinadamu, vyama vya kiraia, maofisa wa serikali na wale wa Umoja wa Mataifa, wakimwemo wanaotoka katika Idara ya Huduma kwa Wakimbizi katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo jijini Dar es

***Continues on Page 3***



Kikundi cha vijana kutoka Kongo wakitoa burudani katika Siku ya Wakimbizi Duniani jijini Dar es Salaam.
**PICHA | UNHCR Tanzania**



Bidhaa za kujikimu zilizotengenezwa na wakimbizi kutoka Burundi zikiwa kwenye maonyesho wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Duniani katika Kambi ya Mtendeli, Wilaya ya Kibondo, Mkoa wa Kigoma.
**PICHA | Winnie Kweka/UNHCR**

Salaam, Mkurugenzi wa Huduma za Wakimbizi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani, Bw. Harrison Mseke, alionyesha kwamba kuna tatizo kubwa la kupungua kwa fedha kwa ajili ya kuwahudumia wakimbizi na alitoa wito kwa wadau kuwawezesha wakimbizi kuishi maisha yenye hadhi na kuendesha kambi za wakimbizi.

Hotuba ya Bw. Mr. Mseke ilisomwa kwa niaba yake na Mratibu wa Mazingira katika Kambi za Wakimbizi katika Wizara ya Mambo ya Ndani, Bw. Thobias Sijabaje. Alisema, kati ya mwaka 2016 na 2018, Tanzania ilipokea pungufu kidogo ya asilimia 26 ya jumla ya mahitaji yote kwa ajili ya kuwasaidia wakimbizi. Alisema kwamba sekta zinazopata fedha pungufu sana ni pamoja na maji, usafi wa mazingira, afya, elimu na mahitaji ya chakula. Bw. Mseke alitoa wito kwa UNHCR na jamii ya kimataifa kuisaidia zaidi Serikali ya Tanzania na ile ya Burundi kuendesha zoezi la kuwarudisha makwao wakimbizi waliohiyari kurejea makwao kutoka katika awamu ya uwezeshaji hadi katika ile ya utekelezaji ili kufikia lengo la kuwarejesha wakimbizi 82,000 hapo ifikapo Desemba 31, 2018.

Akisoma taarifa kutoka kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bw. Antonia Guterres, Mratibu Mkazi wa UN Tanzania, Bw. Alvaro Rodriguez, alinukuu “Nina mashaka makubwa sana kuona kwamba wakimbizi wengi zaidi hawapati kinga wanayoihitaji na ambayo ni haki yao. Tunahitaji kujenga uadilifu wa mfumo wa kimataifa wa kinga ya wakimbizi”. Bw. Rodriguez alisema kwamba jamii ya mahalia na ya kimataifa hazina budi kushirikiana na kujenga umoja ili kusaidia kupatikana kwa mahitaji ya wakimbizi.

Kwa upande wake, Naibu Mwakilishi wa UNHCR, Bi. Joan Allison, alitoa shukrani zake kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watu wa Tanzania kwa kuwapokea wakimbizi wakiwa katika makundi makubwa.

# UN yashinda nafasi ya kwanza katika kundi lake Maonyesho ya Sabasaba




Mtaalamu wa Mawasiliano wa UNICEF, Bi. Usia Nkhoma-Ledama (katikakati kulia) akipokea tuzo kwa niaba ya Umoja wa Mataifa Tanzania kwa kushinda nafasi ya kwanza katika kundi la Taarifa, Uchapishaji kutoka kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa (katikati kushoto) wakazi wa uzinduzi wa Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya arobaini na mbili. **PICHA | Grace Mongi/UNRCO**

Ikiongozwa na Kikosi Kazi cha Mawasiliano cha Umoja wa Mataifa (UNCG), kundi la maofisa mawasiliano wa mashirika ya Umoja wa Mataifa, UN Tanzania ilishiriki katika Maonyesho ya 42 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayojulikana pia kama Sabasaba. Mwaka huu, banda la UN lilishinda tuzo ya kwanza katika kundi la Taarifa, Uchapishaji, Upigaji Chapa na Vifaa vya Ofisini ambalo lilishindanisha taasisi kama ivle Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kampuni ya Magazeti ya Tanzania Standard Newspapers (TSN).

Tuzo hiyo ilikabidhwa na Waziri Mkuu, Mh. Kassim Majaliwa, wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya Sabasaba na ilipokelewa na Mtaalamu wa Mawasiliano wa UNICEF, Bi. Usia Nkhoma-Ledama, kwa niaba ya familia ya UN. Katika maonyesho ya mwaka huu, msisitizo katika banda la UN ulikuwa kutangaza matokeo ya kazi ya UN na kuhamasisha Ubunifu kwa ajili ya Maendeleo Endelevu kwa kuonyesha vijana watatu wabunifu katika banda la UN. Mmoja wa wabunifu hao ni Gracious Fanuel kutoka mkoani Kilimanjaro ambaye ameunda mkono wa kiroboti kwa kutumia vitu vya kawaida vinavyopatikana nyumbani. Mkono huo unaweza kuendeshwa kwa kutumia simu ya mkononi na anatumaini kwamba ataweza kupanua ubunifu huo hadi kuweza kubeba mashine au vitu vikubwa katika mnyororo wa uzalishaji na pia kuwasaidia watu wenye ulemavu. Kijana mwingine mbunifu ni Latifa Mohammad kutoka Zanzibar ambaye aliunda mfumo unaojiendesha wa umwagiliaji maji kwa kutumia ving'amuzi vinavyomaizi ikiwa eneo fulani la ardhi lina maji au la na kuelekeza maji katika eneo hilo lililo kavu. Mfumo huu unafaa kwa sababu kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia 80 ya nguvukazi nchini Tanzania.

Mwisho, alikuwa Amos Mtambala kutoka Dar es Salaam anayetumia ujuzi wake wa sanaa katika ujasiriamali. Amos alipata mafunzo kwa msaada wa ILO na tangu hapo amepanua mtandao wake kiasi cha kuwajumuisha vijana zaidi ya 100 ambao hutengeneza kazi za sanaa na kuziuza nchini na kimataifa. Kulikuwa na mashindano ya ubunifu katika banda ambapo aidi ya watu 500 pale bandani Sabasaba na kupitia mtandao wa kijamii walipiga kura kuamua nani walifikiri ni mbunifu bora zaidi. Mshindi wa jumla alikuwa Latifa ambaye alipata shilingi milioni 3, wa pili alikuwa Gracious Fanuel aliyepata shilingi milioni 2 na wa tatu alikuwa Bw. Amos Mtambala aliyejipatia shilingi milioni 1.

Akizungumza katika banda hilo wakati wa kuwatangaza washindi, Mtaalamu wa Mawasiliano wa UN, Bi. Hoyce Temu, alitoa pongezi kwa vijana akisisitiza kwamba "Mada ya kuhamasisha ubunifu ilichaguliwa kwa makusudi ili kuunga mkonoSerikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kwamba ndoto yake ya maendeleo ya viwanda inafikiwa. Kwa kuzingatia kwamba vijana wanafanya asilimia 55 ya watu Tanzania, ni muhimu kwamba wawe sehemu ya maendeleo leo, kisho na katika siku zijazo."




Mkutubu kutoka UNIC, Bi. Harriet Macha (kushoto), akikabidhi taarifa kuhusu kazi a UN nchini Tanzania kwa Rais mstaafu Jakaya Kikwete (kulia) alipokamilisha ziara yake katika banda la maonyesho la UN.
**PICHA | Grace Mongi/UNRCO**




Washindi wa mashindano ya ubunifu ya UN, Bi. Latifa Ngea (katikati), Gracious Fanuel (kushoto), na Amos Mtambala (kulia), pamoja na Mtaalamu wa Mawasiliano ya Umma wa UN, Bi. Hoyce Temu (nyuma), walishinda kwa kupigiwa kura na zaidi ya watu 500 wengine kwa kwenda kwenye banda na wengine kwa kutumia njia za kielektroniki kumchagua yule waliyeamini ndiye mshindi bora zaidi. **PICHA | Grace Mongi/ UNRCO**




Mtaalamu wa Mawasiliano Umoja wa Mataifa, Bi. Hoyce Temu (kulia) akimshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Masharik, Mh. Dkt Augustine Mahiga kwa kutembelea banda la UN na akimkabidhi taarifa ya nyongeza kwa kazi ya kwa UN nchini Tanzania. **PICHA | MOFAEC**




Afisa Habari wa UNIC, Bi. Stella Vuzo (katikati) akimkabidhi Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mh. Charles Mwijage (kushoto), taarifa kuhusu kazi za Umoja wa Mataifa nchini Tanzania. **PICHA | Aidan Riwa/ UNRCO**

# UN na TEF zawafikiwa waandishi wa habari katika maeneo yao Kigoma




Wahariri Waandamizi wakiwa katika Dawati la Jinsia na Watoto katika Wilaya ya Kasulu ambalo lilianzishwa maalumu kwa ajili ya ushirikana na halmashauri (kutoka kushoto kwenda kulia) Bw. Salehe Mohamed (Tanzania Daima); Bi. Joyce Shebe (Clouds Media); na Bw. Joseph Mwendapole (Nipashe).

***Picha zote na Edgar Kiliba/UNRCO***

Katika kipindi chote cha mwezi uliopita, Umoja wa Mataifa na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) zimekuwa zikiendesha mafunzo kwa waandishi wa habari katika kanda za magharibi na kusini mwa Tanzania. Mafunzo haya ni hatua ya hivi karibuni katika ushirikiano kati ya Kikosi Kazi cha Umoja wa Mataifa cha Mawasiliano (UNCG). Hili ni kundi la maofisa mawasiliano ya umma kutoka katika mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini Tanzania. Ushirika huu na TEF umedumu kwa zaidi ya miaka mitano ambapo kila mwaka wahariri kutoka vyombo vya habari hukutana na kujadiliana na wakuu wa mashirika ya Umoja wa Mataifa kuhusu hatua za maendeleo zinazopigwa na Umoja wa Mataifa na hali ya tasnia ya habari nchini Tanzania.

Malengo ya kutoa mafunzo hayo ni kuwafikia waandishi wa habari katika maeneo yao na kuwapa zana za kuwawezesha kuwa sauti ya wanyonge kwa kuangazia mipango bora ya maendeleo na changamoto za wale walioachwa nyuma. Suala hili limefikiwa kwanza kwa kwenda na wahariri na waandishi wa habari katika maeneo yaliyoteuliwa ambako UN inafanya jitihada katika mikoa husika kabla ya kuendesha warsha ambayo kwayo waandishi wanapata mafunzo kuhusu Malengo ya Dunia na shughuli za UN na matunda yanayopatikana katika mikoa inayohusika na vile vile vipengele vya Uandishi wa Habari wa Kujali Maslahi ya Umma.

Mafunzo ya kwanza yalifanyika katika ukanda wa magharibi. Yalifanyika katika Mkoa wa Kigoma na kuwahusisha waandishi kutoka mikoa ya Geita, Tabora, Kagera, Kigoma na Katavi. Ujumbe wa UN na ule wa TEF ulitembelea miradi mitatu ya UN iliyo sehemu ya Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) katika wilaya ya Kasulu. Mashirika ya UN yanatoa msaada kwa jamii za mkoani Kigoma kwa upande wa kutoa ujuzi na kujenga uwezo, ujasiriamali wa wanawake na kinga ya mtoto.

Miongoni mwa maeneo yaliyotembelewa ni pamoja na Kituo cha Huduma Mbalimbali za Jamii kilichojengwa na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) kupitia fedha zilizotolewa na Norway na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi kilichoanzishwa na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA). Vijana na wanawake katika vituo hivi hujifunza ujuzi muhimu kuhusiana na ujasiriamali na teknolojia ya habari na mawasiliano, miongoni mwa mada mbalimbali. Ujumbe pia ulitembelea kikundi cha wanawake wajasiamalia waliopata mafunzo kutoka Shirika la UN la Wanawake kuhusu namna bora ya kuendeleza biashara zao ikiwemo kupat amikopo, namna ya kuuza bidhaa zao na kupat masoko.

Vilevile walitembelea mfumo wa kinga kwa watoto unaofadhiliwa na UNICEF, ambao unahusisha Dawati la Jinsia na Watoto na pia ‘Familia za Malezi’ na nyumba za watoto. Huu ni utaratibu mbadala kwa ajili ya watoto ambao kwa sababu moja au nyingine hawawezi kuishi na wazazi wao.

Mratibu wa eneo kwa upande wa Kigoma, Bw. Evance Siangicha, alisema kwamba miradi hii ilikuwa ni baadhi ya matokeo ya mipango inayosimamiwa na UN kama sehemu ya KJP na kwamba kuna mingine mingi inapangwa kwani KJP ndiyo kwanza imetimiza mwaka mmoja. “Tayari tunaweza kuona kwamba jamii za wenyeji wananufaika kutokana na kazi za

***Inaendelea Ukurasa8***

## Ziara ya Kigoma

*Kutoka Ukurasa8*

mashirika ya UN. Hili linawezeshwa na serikali ya Norway na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA)," alisema Bw. Siangicha. Kwa ufadhili wa Serikali ya Norway, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA) na Serikali ya Sweden, Mpango wa KJP unahusisha mashirika 16 ya Umoja wa Kimataifa yanayojishughulisha katika maeneo sita ambayo ni nishati na mazingira endelevu; uwezeshaji vijana na wanawake kiuchumi; ukatili dhidi ya wanawake na watoto; elimu kwa kuwazingaita wasichana walio katika umri wa balehe; Maji, Usafi wa Mazingira na Usafi wa mwili (WASH); na Kilimo.



Waandishi wa habari kutoka Mkoa wa Kigoma, Bi Edith Karlo (kushoto), Bi Happiness Tesha (kulia) na Mheshimiwa Deogratius Nsokolo wakimhoji Afisa wa Wilaya ya Kasulu, Bw. Simon Kazzo, baada ya kuambiwa kuhusu jinsia na Desk ya Watoto.



Wahariri na waandishi wa habari wakiwa ndani ya moja ya madarasa ambapo UNHCR na Ujirani Mwema, Asasi ya Korea wakitoa mafunzo katika kituo cha MCC, eneo la kujifunzia kuchakata sabuni. Madarasa katika kituo cha MCC yamejengwa na wenyeji kwa kushirikiana na wakimbizi

# Ripoti Maalum
# Ujumbe wa UN, TEF watembelea miradi iliyo mikoa ya Lindi na Mtwara



Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez (kushoto) na Katibu wa TEF, Bw. Neville Meena (kushoto kwake) wakijaribu kutumia pampu ya maji iliyofunguwa katika Seminari Ndogo ya Rondo. Kwa msaada wa UNDP, shule imeimarisha mfumo wake wa kukusanya maji na hivi sasa ina matenki matatu ambayo yanaweza kuhifadhi hadi lita 600,000 za maji. *****Picha zote na Edgar Kiliba/UNRCO***

Katika awamu ya pili ya Mafunzo kwa Waandishi wa Habari katika Kanda, mikoa ya kusini mwa Tanzania ilifikiwa. Warsha ilifanyika katika Mkoa wa Mtwara ambapo ilihudhuriwa na waandishi kutoka Pwani, Ruvuma, Lindi na Mtwara.

Mkoani Lindi, ujumbe uliohusisha maofisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ulimtembelea Mkuu wa Mkoa, Bw. Godfrey Zambi, kabla ya kutembelea miradi miwili iliyo mkoani humo. Wa kwanza ni ule unaowasaidia wakulima na wazalishaji wa chumvi kuhakikisha kwamba chumvi yao inawekwa kiasi cha kutosha cha madini joto. Madini joto ni muhimu sana kwa ukuaji wa ubongo kwa watoto na hupunguza hatari zinazotokana na ujauzito. Tangu mwaka 2015, mradi umetoa msaada wa Shilingi milioni 978 kwa wazalishaji wadogo 200 wa chumvi ambayo imewafikia takribani watu milioni 1.8 katika mikoa ya Lindi na Mtwara wanaotumia chumvi hiyo kila siku.

Mradi wa pili ni ule wa UNDP wa kusaidia jamii Kuendana na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi. Mradi huo ulianza mwaka 2015 na umesaidia takribani paneli 20 za umeme wa jua kuunganishwa katika Seminari Ndogo ya Rundo na katika kituo kimoja cha afya. Pia umeweza kujenga matenki matatu ya kuhifadhia maji katika shule na kituo cha afya. Matenki hayo yana uwezo wa kuhifadhi lita 600,000 za maji. Zaidi ya vikundi 20 vya akina mama pia vimepata misaada kwenye shughuli zao kama vile ufugaji kuku na kilimo cha alizeti. Mradi huo umewaletea matokeo mazuri zaidi ya watu 3,000 kwa bajeti inayokadiriwa kuwa shilingi milioni 500.


Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, alitoa pongezi kwa miradi hiyo na kuelezea jinsi ilivyoleta matokeo mazuri katika maisha ya watu. "Upungufu wa madini joto ni tatizo ambalo halizungumziwi sana lakini linaweza kuleta madhara makubwa katika afya za watu. Kazi ambayo UNICEF inafanya kwa kushirikiana na serikali kuongeza uzalizhaji wa chumvi yenye kiasi cha kutosha cha madini joto ni ya kupongezwa," alisema Bw. Rodriguez. Vilevile alitoa pongezi kwa mradi wa UNDP wa kuwasaidia watu kuendana na mabadiliko ya tabia ya nchi akieleza kwamba, "Kutokana na Madhara ya mabadiliko ya tabia ya nchi hatuna budi kuleta ufanisi zaidi katika namna tunavyoleta maendeleo, kwa hiyo, paneli za nishati ya jua na miundombinu yake ambayo UNDP imefunga katika kituo cha afya na shule katika Kijiji cha Ngala inaonyesha kwamba ufumbuzi endelevu kwa nishati unaweza kuongeza ubora wa maisha ya watu."

"Mradi wa UNDP ni miongoni mwa miradi bora kabisa katika ile tuliyotembelea. Afya, nishati, uwezeshaji wa kiuchumi, ujasiriamali, maji safi na salama, elimu na kilimo, yote yanatekelezwa vema katika kijiji kimoja," alisema Katibu wa TEF, Bw. Neville Meena. "Unaweza kuona waziwazi matokeo chanya ya miradi hii katika nyuso za wanakijiji na watoto wenye afya na furaha."

Mkoani Mtwara, ujumbe wa maofisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, UN na TEF na waandishi wa habari kutoka Mtwara walimtembelea Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kabla ya kutembelea Mradi wa Usajili Vizazi wa UNICEF. Huu ni mradi kwa ajili ya wtoto wa chini ya miaka mitano mkoani Mtwara. Tangu utekelezaji wake uanze mwaka jana, takribani watoto 170,000 wamesajiliwa mkoani humo sawa na asilimia 94 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mwaka 2017. Mradi huo pia umekuwa ukitekelezwa mkoani Lindi tangu mwaka jana ambapo watoto 120,000 walisajiliwa, sawa na asilimia 101 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika mwaka 2017.



Mhudumu anayefanya kazi katika Zahanati ya Ziwani, Bi. Constansia Kalambo, akimsajili mtoto. Mara baada ya kuchukua taarifa za mtoto, Bi. Kolambo anatuma taarifa hizo hadi ofisi ya RITA ya wilayani ambapo itapitishwa na mtoto anapewa cheti cha kuzaliwa.



Paneli ishirini za umeme wa jua zimefungwa katika kila moja ya jengo la shule na kliniki.



Mzalishaji wa chumvi kutoka Mkoa wa Lindi akizungumza na waandishi wa habari kuhusu msaada aliouptokea kutoka UNICEF. Alipewa mafunzo na vifaa ili kuhakikisha kwamba chumvi anayozalisha inakuwa na madini joto ya kutosha.

# Watoto wapatiwa huduma za dharura katika Mkoa wa Kigoma



Kutoka Kushoto kwenda Kulia: Bw. Kapaya – Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya, Halmashauri ya Mji wa Kasulu; Ophilia Karumuna – Mtaalamu wa Kinga ya Watoto nykati za Dharura, UNICEF Kibondo, Sophia Kamali, mtu mwema; Mbelwa Gabagambi—Mtaalamu wa Kinga ya Watoto (Kusimamia kesi), Ofisa wa UNICEF; na Bw. Wabike – Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya, Halmashauri ya Kasulu Mjini. **PICHA | UNICEF Tanzania**

Bi. Sophia Kamali, mwanamke aliyeolewa na mama wa watoto wawili wenye umri wa miaka 24 na 13, anaishi katika eneo tulivu la mji wa Kasulu, Mkoa wa Kigoma. Anafanya kazi katika AZISE ya mahalia kama bibi afya ambaye kazi yake ni kutoa elimu kuhusu afya ya uzazi. Katika muda wake wa ziada, anafanya kazi katika bustani yake ya mbogamboga na hujitolea kama mwezeshaji katika mikutano ya wazazi ya kutoa elimu kuhusu malezi bora.

Bi. Kamali ni miongoni mwa 'Watu Wema' 11 katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu walio katika mfumo wa kinga ya watoto, ambao wamewezeshwa na halmashauri kupitia UNICEF. 'Watu Wema', katika baadhi ya nyakati, 'Familia Njema' (kwa wale walio kwenye ndoa), wanatoa matunzo ya familia wakati wa dharura kwa watoto ambao hawaezi kukaa na wazazi wao kwa sababu kama vile ukatili, kushindwa matunzo, au kutelekeza. Njia hii ya matunzo ya muda ni sehemu ya usimamizi wa mashauri chini ya Ofisa wa Ustawi wa Jamii wa Wilaya.
Kamali alifiwa na mama yake alipokuwa na umri wa mwaka mmoja tu. Yeye na mdogo wake wa kike aliyekuwa na miezi 7 walibaki na baba yao ambaye hakumudu kuwatunza. Wasichana hao walitunzwa na wanaukoo mbalimbali katika mazingira duni huku kukiwa na chakula kidogo tu."Ninaelewa yale ambayo watoto wanapitia katika mazingira ya unyanyasaji, au pale wazazi wanaposhindwa kumudu matunzo, au pale wanapotelekezwa, maana nami nimeyapitia hayo," anasema Kamali. Kwa miaka minne sasa, ametoa matunzo kwa watoto 26 nyumbani kwake.

Mpango wa Familia Njema uliingizwa katika mfumo wa kinga ya mtoto wa Halmashauri ya Mji wa Kasulu kabla ya utekelezaji wa Programu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) ambao hivi sasa ni sehemu ya matokeo ya eneo la Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (VAWC). Tangu kuanzishwa kwa Programu ya Pamoja ya Kigoma mwaka 2017, Familia Njema 56 zimetoa matunzo kwa watoto 117 katika Wilaya ya Kasulu (Halmashauri ya Mji wa Kasulu, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Wilaya ya Kibondo na Wilaya ya Kakonko).

Familia Njema zinasajiliwa na kupewa mafunzo na Maofisa wa Ustawi wa Jamii wa Wilaya wakitumia miongozo na mafunzo yaliyoandaliwa nwa Idara ya Ustawi wa Jamii (Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto). Msaada wa kifesha hutolewa kwa watu wema ili kuwasaidia watoto katika matunzo yao.



Wahariri na waandishi wa habari wakikutana na Mama Sophia (kulia kabisa) ambaye alipata mafunzo na msaada wa kifedha kutoka serikalini kupitia UNICEF, ili kutoa uangalizi wakati wa dharura. Mama Sophia katika familia njema za Kibondo, Kasulu na Kakonko. Mama Sophia ni miongon mwa 'Kaya Njema' za Kibondo, Kasulu na Wilaya ya Kakonko. Kwa ujumla familia hizo zimewaangalia zaidi ya watoto 117.
**PICHA | Edgar Kiliba/UNRCO**

# Programu ya Ufadhili kwa Wanafunzi Wakimbizi yafufua matumaini ya wakimbizi nchini Tanzania



Hawa ni wakimbizi wa mwanzo (Wakongo 2; Warundi 3) waliotoka katika kambi baada ya kushinda tuzo ya kwenda masomoni kutoka katika Programu ya Wanafunzi Wakimbizi ambayo inayosimamiwa na World University Service of Canada (WUSC). **PICHA | UNHCR Tanzania**

Anderson, ambaye ni mkimbizi kutoka Kongo anayeishi katika Kambi ya Nyarugusu, Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma, ana ndogo ya kuwa mwanaharakati wa Haki za Binadamu na pengine, siku moja, kufanya kazi Umoja wa Mataifa. Leo, ana matumaini makubwa zaidi kwani amepiga hatua kuelekea kutimiza ndoto yake hiyo baada ya kupata ufadhili chini ya Programu ya Msaada wa Elimu kwa Wanafunzi Wakimbizi na atakwenda kusoma katika chuo kikuu nchini Kanada mwezi Septemba.

Anderson ndio kwanza alikuwa amehitimu elimu ya sekondari katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo wakati alipolazimika kuyakimbia makazi yao na kuja kutafuta hifadhi nchini Tanzania mwaka 2013. Kama wakimbizi wengine wengi, alikuwa mhanga wa ukatili na mateso katika nchi yake ya asili. "Nataka kusoma Sheria ya Sanaa katika Uhusiano wa Kimataifa au Sheria," alisema Anderson. Yeye ni mmoja kati ya wanufaika watano nchini Tanzania kupitia Programu ya Msaada wa Masomo kwa Wanafunzi Wakimbizi (SRP) inayosimamiwa na taasisi ya World University Service of Canada (WUSC).

SRP husaidia zaidi ya wanafunzi wakimbizi 130 kila mwaka kutoka pahali mbalimbali duniani na kuwapa fursa zinazobadilisha maisha yao kwa kuendelea na elimu yao katika vyuo vikuu nchini Kanada. Emery ni mkimbizi kutoka Burundi na ambaye pia ni mnufaika wa programu ya WUSC. Emery alifiwa na wazazi wake wote wawili wakati wa machafuko ya kisiasa nchini Burundi. "Nilikuwa shuleni katika jimbo/mkoa mwingine nilipopata taarifa hizo kuhusu familia yangu," Emery alivuta kumbukumbu. Wazazi wake wote wawili walikuwa walimu nchini Burundi na wanachama wa chama cha upinzani. "Baada ya wazazi wangu kufariki dunia, nilijua kwamba nilipaswa kuondoka Burundi," aliendelea kusimulia Emery.

Emery aliamua kuwaenzi wazazi wake kwa kuwafundisha watoto pale kambini Lugha ya Kiingereza. Ndoto yake ni kuwa kionozi lakini hutumia muda wake kufundisha wanafunzi wa darasa la 3 na 4 Lugha za Kifaransa na Kirundi katika Shule ya Msingi Nuru.

Mpango wa Kusimamia Elimu kwa Wakimbizi wa UNHCR hutafuta kutoa upatikanaji ulio wa usawa wenye haki, elimu rasmi na elimu mbadala kwa watoto wa shule za awali, msingi na sekondari. Licha ya kutumia njia ya kuwa na awamu mbili za masomo kwa siku, bado upungufu wa madarasa unafanya watoto wanaendelea kusomea chini ya mti. Kuna upungufu wa matini ya kufundishia na kujifunzia jambo linaloathiri vibaya uandikishwaji na watoto kuendelea kubaki shuleni. Hivi sasa, ni asilimia 78 tu ya watoto wa umri wa kwenda shule za msingi ndio wanaohudhuria shuleni, ambapo wengi wao wanasomea chini ya miti. Kiasi cha Dola za Marekani 800,000 kinahitajika ili kukabili pengo hili katika mwaka 2018.

> *"Nataka kusoma Sheria ya Sanaa katika Uhusiano wa Kimataifa au Sheria,"*
>
> **Andersone Mwanafunzi Mkimbizi aliye nufaika na mpango wa Umoja wa Mataifa**

## Waziri Mkuu azindua Kampeni ya VVU ya 'Furaha Yangu'



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa, akiongoza kampeni ya kupima VVU mkoani Dodoma. Kampeni hiyo inatambulika kwa jina la 'Furaha Yangu'. ***PICHA | ILO Tanzania***

Mwezi Juni, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kassim Majaliwa, alizindua kampeni ya nchi nzima ya kupima VVU huko Dodoma. Ikiwa imepewa jina la 'Furaha yangu', kampeni inalenga kuwahamasisha Watanzania wote, hasa wanaume na vijana kwenda kupima na kuanza tiba mapema endapo watakuwa na VVU. Waziri Mkuu, aliwaasa watu kushiriki kampeni na alisema kwamba serikali inajaribu kufikia lengo la dunia la 90-90-90 ifikapo mwaka 2020. Hii ina maana kwamba ifikapo mwaka 2020, asilimia 90 ya watu wote wanaoish na VVU wawe wamejua hali yao, asilimia 90 ya waliokutwa na VVU wawe wakipata tiba na asilimia 90 wawe wameshinda kudidimiza virusi mwilini mwao.

Kupitia Programu ya Pamoja ya VVU na UKIMWI ya UN, Shirika la Kazi Duniani (ILO) na UNAIDS yanashirikiana na serikali, washirika wa kijamii na wadau wengine kutekeleza kampeni ya Furaha Yangu ili kuhamasisha jamii, hasa wanaume, kujua hali zao za VVU kama msingi wa kuanza tiba mapema na kuzuia.
Waziri Mkuu alionyesha masikitiko yake kuwa hadi sasa, ni asilimia 45.1 tu ya wanaume walioambukizwa VVU ndio wanaojua hali yao kulinganisha na asilimia 55.9 (umri kati ya miaka 15 – 64). Aliongeza kwamba kwamba watu wapatao milioni 1.4 wameambukizwa VVU, hii ikiwa ni sawa na asilimia 4 ya idadi ya watu milioni 54.2 nchini.

"Jitihada zifanyike sasa kuwalinda asilimia 95 waliobaki ili wasiambukizwe na pia kuwalinda hawa asilimia 5 ili walipatwe na maambukizo mapya na hatimaye mauti," alisema. Alitoa maagizo kwa Wakuu wa Mikoa wote na Mawaziri kushirikiana na wadau wa VVU/UKIMWI ili kutoa elimu kwa watu katika mikoa na wizara zao kujitokeza kupima na kuanza tiba mapema endapo watakutwa wameambukizwa.

Katika tukio hilo, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera, Masuala ya Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mh. Jenista Mhagama, aliwapongeza wadau wote wakiwemo ILO, UNAIDS, USAID na wengineo kwa kuunga mkono juhudi za Serikali za kupambana na janga hilo.

Alisisitiza kwamba kampeni hiyo siyo tu itato idadi kamili ya watu walioambukizwa VVU, bali itasaidia nguvu kazi ya taifa kuleta tija zaidi katika maendeleo ya nchi. Aliongeza kwamba vijana walikuwa ndio kundi la kidemografia lililoathirika zaidi.




# "Ni muhimu kufanya juhudi ili kuwalinda asilimia 95 ya watu wasio na maambukizi na pia kuwalinda asilimia 5 wenye maambukizi wasipate maambukizi mapya na hatimaye kifo"

Mh. Waziri Mkuu, Bw. Kassim Majaliwa.

## Siku za Umoja wa Mataifa:

**30 Julai – Siku ya Dunia ya kupinga Usafirishaji Haramu wa Wanadamu**
**12 Agosti – Siku ya Kimataifa ya Vijana**
**19 Agosti – Siku ya Kimataifa ya Misaada ya Kibinadamu**

***Umoja wa Mataifa Madhubuti kwa Dunia Bora Zaidi !***

### Mabadiliko ya UN kwa ufupi

Tanzania ni moja kati ya nchi zinazoongoza katika mpango wa kufanya kazi pamoja. Tangu Julai 2016, timu ya wakuu wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa Tanzania wamekuwa wakiufanyia kazi mpango. Mpango wa Umoja wa Mataifa wa kusaidia Tanzania (UNDAP II). Kwa taarifa zaidi kuhusu mipango na mapitio ya UN tembelea: **www.undg.org**

United Nations TANZANIA Delivering as One

**UN Resident Coordinator's Office**

**Communications Specialist**

hoyce.temu@one.un.org

Phone : (+255) 22-219-5021



**Kwa taarifa zaidi tembelea: tz.one.un.org**